# JARIDA LA USHIRIKA

ISSN 2714-2175 Toleo Na: 007 JULAI – SEPTEMBA, 2021



## "DHAMIRA YA SERIKALI NI KUIMARISHA USHIRIKA ILI KUINUA UCHUMI WA MWANANCHI" – WAZIRI MKUU





"Ushirika – Pamoja Tujenge Uchumi"

# JARIDA LA USHIRIKA



"Ushirika – Pamoja Tujenge Uchumi"

## YALIYOMO


- Kutoka kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania....3
- Serikali imedhamiria kuimarisha Ushirika - Waziri Mkuu ....4
- Wakulima wa Zabibu wahamasishwa kujiunga na Ushirika....6
- Waziri Mkenda awataka Maafisa Ushirika kusimamia Vyama kwa ufanisi....9
- Kikao cha wadau kujadili mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013....12
- Ushirika watakiwa kujiendesha kisasa na kugusa makundi yote....14
- Warajis Wasaidizi watatu wabadilishiwa vituo vya kazi, mmoja ateuliwa....17
- Wito watolewa Ushirika kuongeza kasi ya Viwanda....19
- Kamati Maalum ya Bunge yafanya Ziara katika mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara ili kujifunza namna Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unavyotekelezwa....22
- Shirika la USADF limetoa Shilingi millioni 231.6 kwa Ushirika wa Wakulima wa Maparachichi, Rungwe....24
- Vyama vya Ushirika na Maafisa Ushirika Mkoani Rukwa wapata vitendea kazi....26
- Mnada wa kwanza wa Mbaazi Tunduru waingiza Shilingi 466,623,690.00....27
- Makala za Ushirika wa Nyumba....29
- Ushiriki wa TCDC katika Maonesho ya Biashara ya 45 ya Sabasaba, Dar es Salaam....32
- Ushiriki wa TCDC katika Maonesho ya 16 ya Biashara ya Afrika Mashariki Mkoani Mwanza

# KUTOKA KWA MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA NA MTENDAJI MKUU WA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA

**Ndugu wasomaji,,**

Niwakaribishe tena katika Jarida la Ushirika Toleo la saba, ambalo ni mfululizo wa majarida yanayoandaliwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania katika jitihada za kuelimisha na kuhamasisha masuala na hatua mbalimbali zinazofanyika katika Sekta ya Ushirika.



***Dkt. Benson Ndiege, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)***

Kama mnavyofahamu Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuendeleza na kuimarisha Ushirika ili kuhakikisha kuwa Vyama hivi vinaendelea kuongeza tija na mchango mkubwa kiuchumi. Katika kutekeleza azma hii tayari Tume ya Maendeleo ya Ushirika ipo katika hatua za kiutendaji za kuimarisha zaidi matumizi ya Mifumo ya Kieletroniki katika ukusanyaji wa taarifa ambazo zitasaidia Ushirika kujiendesha kisasa. Aidha, Mifumo hiyo itasaidia katika uendeshaji na usimamizi bora wa Vyama vya Ushirika, utunzaji wa takwimu pamoja na kumbukumbu za Ushirika.

Kupitia ziara mbalimbali za Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa katika mashamba na Vyama vya Ushirika hasa vinavyojishughulisha na zao la Zabibu mkoani Dodoma, tunaendelea kuona dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuhakikisha kuwa Vyama vyaUshirika vinaimarika kiutendaji na vinakuwa chachu ya uzalishaji wa malighafi za viwandani.

Sambamba na hilo Tume tayari imechukua hatua ya kuhakikisha kuwa inawajengea uwezo Maafisa Ushirika katika usimamizi na ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Tume imeandaa na inatekeleza programu maalum ya mafunzo kwa Maafisa Ushirika nchini ambapo kupitia mafunzo hayo watapata fursa ya kujifunza na kuelewa masuala ya msingi ya kiusimamizi wa Vyama vya Ushirika. Miongoni mwa mambo muhimu katika mafunzo hayo ni pamoja na masuala ya uandishi sahihi wa vitabu, ukaguzi wa vyama, udhibiti wa ndani, taratibu za usajili na ufilisi, utatuzi wa migogoro na Sheria ya Ushirika. Hivyo basi, hizi ni baadhi ya hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Tume katika kuhakikisha Vyama vinakuwa imara na endelevu.

***Karibuni sana!***

## SERIKALI IMEDHAMIRIA KUIMARISHA USHIRIKA - WAZIRI MKUU

Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) amesema Serikali ya Awamu ya Sita ina dhamira ya dhati kuhakikisha kuwa Vyama vya Ushirika vinaimarika na wakulima wanapata tija na manufaa katika shughuli za uchumi zinazoendeshwa kwenye Vyama vya ushirika.

Hayo yamesemwa na Waziri Mkuu katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani Julai 03, 2021 kwenye viwanja vya Nanenane mkoani Tabora.



***Mhe.Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (Mb) akihutubia wanaushirika wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani, mkoani Tabora***

Mhe. Kassim Majaliwa ameeleza kuwa Ushirika ni Sekta muhimu yenye mchango mkubwa kwa Taifa ambayo inahusisha shughuli za uchumi ikiwemo Kilimo, Uvuvi, Ufugaji na Nyanja nyingine za uchumi ambazo zote hutoa ajira na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa. Hivyo, amewataka Viongozi na watendaji wa Sekta ya Ushirika kuhakikisha kuwa Vyama vya Ushirika vinaendeshwa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu, na kusimamia Vyama kwa misingi ya uadilifu ili kuondokana na changamoto ambazo zimekuwepo zinazoharibu taswira ya Ushirika.

“Lazima tuzilinde mali za Ushirika jukumu tulilonalo viongozi wa Ushirika ni kusimamia mali za Ushirika na kuheshimu dhamana tulizopewa na wanaushirika,” alisema Waziri Mkuu Akizungumzia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala Waziri Mkuu amesema mfumo huo ni mkombozi kwa wakulima kwani mkulima anapata fursa ya kupata bei yenye ushindani kupitia minada ya ununuzi ambayo mara nyingi ni ngumu kuipata kwa walanguzi. Hivyo, ameitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuendeleza juhudi za kuelimisha kuhusu mfumo huu na kuhakikisha hata maeneo yenye changamoto na mfumo elimu itolewe ili wakulima waelewe manufaa ya mfumo.



***Mhe.Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (Mb), akitembelea mabanda ya Wanaushirika wakati wa kilele cha Maadhimisho ya siku ya Ushirika Duniani mkoani Tabora, Tanzania.***

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege amesema Tume inaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za Awamu ya Sita za kufufua viwanda ili kuongeza thamani za mazao yanayozalishwa na wakulima. Ameongeza kuwa kwa kipindi cha mwaka jana tayari viwanda vitatu vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika vimeanza kufanya kazi akivitaja viwanda vinavyomilikiwa na KACU, Chato na Mbogwe, jambo ambalo linasaidia kuongeza bei ya mazao na ushindani wa soko.

Aidha, Dkt. Ndiege ametoa wito kwa vyama vya Ushirika kuitumia Benki ya Ushirika ya KCBL ambayo tayari imeanza kazi kuanzia Novemba 2020. Mrajis ameongeza kuwa Benki hiyo ni mahususi kwaajili ya wanaushirika na tayari imeanza kupata faida.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) Bi. Theresia Chitumbi alieleza Kauli Mbiu ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika duniani 2021 isemayo “Ushirika tujijenge upya kwa ubora na tija” inalenga kuonesha ustahimilivu wa Vyama vya Ushirika katika kusaidia na kutoa michango ya utu kwa jamii katika kipindi cha majanga mbalimbali kama mabadiliko ya

tabia nchi, uharibifu wa mazingira na hali ya hewa. Kauli Mbiu hiyo inalenga kuchochea vyama vya ushirika kutumia nguvu yake ya umoja, maadili yake na tunu katika kutafuta suluhu ya changamoto.

Mwenyekiti huyo ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuamini Ushirika kama taasisi zenye uwezo wa kuchochea maendeleo ya uchumi pamoja na jitihada kubwa za urejeshaji wa mali za Ushirika zilizokuwa zimeuzwa na kuchukuliwa bila utaratibu zikiwemo nyumba za makazi, maghala, viwanda na viwanja. Akiongeza kuwa wanaushirika wana imani kuwa Serikali itaendelea na zoezi hilo la kutafuta na kuzirudisha mali za ushirika.

Mwenyekiti wa Shirikisho hilo akielezea baadhi ya Changamoto inazozikabili Vyama vya Ushirika wa akiba na Mikopo (SACCOS) amesema Vyama hivi hupokea hisa, akiba, na amana za wanachama kupitia makato ya mishahara ya watumishi husika.

Hata hivyo, fedha hizo hukatwa tozo la gharama (processing fees) kwa asilimia mbili na vyama hupokea fedha pungufu za wanachama kwa kiasi cha asilimia hizo lakini hulazimika kujazia mwanachama fedha kamili kwenye taarifa zake hivyo kusababisha vyama kuingia hasara.

## WAKULIMA WA ZABIBU WAHAMASISHWA KUJIUNGA NA USHIRIKA

Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa (Mb),amesema Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuliongeza zao la Zabibu kuwa miongoni mwa mazao ya kimkakati ili kuongeza thamani zao hilo na tija kwa wakulima. Amewataka wakulima wa Zabibu kuanzisha au kujiunga katika vyama vya Ushirika ili waweze kupata huduma za ughani, upatikanaji wa pembejeo kiurahisi na kupata soko lenye tija kwa mazao yao.

Waziri Mkuu amesema hayo Julai 5, 2021 jijini Dodoma wakati wa ziara ya kutembelea na kukagua shughuli katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Makutopora, Shamba na Kiwanda kidogo cha Mvinyo kilichopo Msalato, Skimu ya umwagiliaji na kiwanda cha CETAWICO Hombolo, Dodoma.



***Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) akikagua Zabibu zinazozalishwa na wakulima wa Vyama vya Ushirika Hombolo, mkoani Dodoma***

Mhe. Majaliwa amesema kuwa dhamira ya serikali ni kuwainua wakulima kupitia zao hilo. Pia Waziri Mkuu amewaeleza wakulima wa Zabibu kuwa Serikali imedhamiria kuboresha kilimo cha zao hilo kwa sababu kilimo ni mkombozi kwa Watanzania.

"Serikaliya Awamu ya Sita imedhamiria kuliongeza zao la Zabibu kuwa miongoni mwa mazao ya kimkakati ili kungeza thamani zao hilo na kuongeza tija kwa wakulima, tunataka kumsaidia mkulima kuanzia maandalizi ya shamba, upatikanaji wa pembejeo hadi hatua ya mauzo." Alisema Waziri Mkuu

Amesema kuwa kampeni hiyo itaanzia mkoa wa Dodoma kwa kuwa Zabibu ni fursa ya kiuchumi nchini na ardhi yote ya Wilaya za Mkoa wa Dodoma inakubali kilimo hicho.



***Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) akikagua shamba la Zabibu Hombolo, Mkoani Dodoma***

Katika hatua nyingine, akizungumza kwenye mkutano wa wadau wa Zabibu, Waziri Mkuu alisema ni muhimu Vyama vya Ushirika hasa vilivyopo mkoani Dodoma kuzingatia taratibu sahihi za kilimo hicho kwa kusaidiana na Maafisa Ugani wa maeneo yao, kuanzisha vitalu vya miche bora katika maeneo ya mashamba ya Ushirika pamoja na masuala ya utawala bora katika uendeshaji wa vyama hivyo.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwemo wamiliki wa viwanda, wakulima, wanaushirika, watendaji wa Serikali, wabunge, taasisi za kifedha, mashirika ya Utafiti wa Kilimo pamoja na wahamasishaji wa zao hilo kutoka maeneo mbalimbali.

"Kilimo cha Zabibu ni kizuri sana mfano yapo maeneo ambayo ni mazuri mno, kama serikali ingejikita katika kuwawezesha wakulima mambo yatakuwa mazuri hata kama una mtaji mdogo unaweza kuanzisha kilimo cha zabibu na utasafisha shamba, utang'oa visiki, utachimba mtaro na utaweka mbolea, baada ya miezi mitatu mvua inapoanza ndiyo unashughulika kwa kupanda miche mpaka mvua itakaposimama na kuacha miche inajiendesha yenyewe," amesema Justine Kuyega, Mkulima wa Zabibu.



***Justine Kuyega, Mkulima wa Zabibu akiwa shambani kwake***

Mkulima wa Zabibu, Salatieli Simule, alisema kilimo cha Zabibu kina manufaa sana mfano heka moja na nusu kipindi cha nyuma kilikuwa kinampatia kipato kidogo kama milioni 6 hadi 7 lakini hivi sasa hekali moja inaweza kutoa tani 14 ambayo ni zaidi ya shilingi milioni 19 hadi 20.

Naye Winifrida Degela, Mkulima wa Zabibu Hombolo, aliwahaamasisha wakinamama kujiunga kwenye kilimo cha Zabibu kwakuwa kina faida sana kutokana na kuvunwa mara mbili kwa mwaka.

Mkulima wa Zabibu, Irene Mlola, aliishukuru Serikali kwakuwa viwanda vingi vya kusindika mvinyo vimeanzishwa na vingine vitaanzishwa ili kukidhi mahitaji ya kuagiza mchuzi nje ya nchi na wenye viwanda kuhakikisha wanachukua zabibu hapahapa nchini



***Irene Mlola, Mkulima wa Zabibu akikagua shamba lake***




*Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) akioneshwa aina mbalimbali za mvinyo kutokana na  zao la Zabibu, wakati wa mkutano wa Wadau wa Zabibu mkoani Dodoma*

## WAZIRI MKENDA AWATAKA MAAFISA USHIRIKA KUSIMAMIA VYAMA KWA UFANISI

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amewataka Maafisa Ushirika nchini kuhakikisha mafunzo ya kuwajengea uwezo yaliyoandaliwa na Tume ya Maendeleo Ushirika Tanzania (TCDC) yanawasaidia kusimamia vyama na kuwahamasisha wakulima wa mazao mbalimbali ikiwemo zao la Korosho kujiunga kwenye Ushirika katika maeneo yao.



***Waziri wa Kilimo Mhe. Prof. Adolf Mkenda akifungua mafunzo kwa Maafisa Ushirika yaliyofanyika Mkoani Mtwara***

Wito huo umetolewa na Waziri wa Kilimo, tarehe 20/09/2021, wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa Maafisa Ushirika yaliyofanyika mkoani Mtwara yenye lengo la kuwajengea uwezo wa kusimamia na kuvikagua vyama, ili kuufanya Ushirika uweze kuimarika na kuwa wa kisasa zaidi. Mafunzo hayo yanafanyika kwa awamu, kwa Maafisa Ushirika wote nchini na yamegawanywa katika Kanda tano ikiwemo Mtwara, Mwanza, Mbeya, Manyara pamoja na Morogoro.

Prof. Mkenda amesema matumaini yake makubwa ni kuona kuwa mafunzo hayo yatakuwa na tija katika kusimamia vyama na hivyo Maafisa hao watakuwa na uwezo wa kuendeleza vizuri Ushirika nchini. Amewataka Maafisa Ushirika watambue kuwa Ushirika siyo wa kukusanya mazao pekee na kumkabidhi mtu mwingine kuuza matokeo yake fedha nyingi za mazao haziendi kwa mkulima na badala yake zinabaki kwa mtu wa kati. Hivyo, amewataka Maafisa Ushirika wavisaidie Vyama vya Ushirika viweze kutafuta Soko la mwisho kwa mazao ya wakulima.

“Haitusaidii sisi kuwa tunalima Korosho, Vyama vyetu vya Ushirika vinakusanya Korosho, halafu anakuja sasa Mtu anachukua Korosho anapelekea India na Vietnam halafu yule wa India na Vietnam anachukua ile Korosho anaitengeneza vizuri anaenda kuuza Marekani anaenda kuuza Ulaya haitusaidii,” alisema Profesa Mkenda.



***Washiriki wa Mafunzo kwa Maafisa Ushirika yaliyofanyika Mkoani Mtwara***

“Tusaidie Vyama vyetu kubangua Korosho na kutafuta Soko la mwisho ili tunapolima Korosho na kuzungumzia mnada anakuja Mtu anachukua Korosho anapeleka nje mkulima hajui bei ya nje halafu huyu wa nje anatengeneza na kuuza nje kwa faida kubwa na mkulima anabaki maskini,” amesema Waziri wa Kilimo.



***Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, akizungumza katika ufunguzi wa Mafunzo kwa Maafisa Ushirika  yaliyofanyika Mkoani Mtwara***

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini na Mtendaji wa Tume ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kujenga ushirika mpya, wa kisasa lakini pia wenye kuaminiwa na wananchi.



***Mmoja wa Wakufunzi Dkt. Jones Kaleshu akitoa Mada katika Mafunzo ya Maafisa Ushirika yaliyofanyika Mtwara***

Dkt. Ndiege amesema kuwa Maafisa Ushirika ndiyo wanaoshughulika moja kwa moja na vyama vya ushirika; hivyo ni muhimu Maafisa hao wakawezeshwa kuwa na uelewa mzuri wa kusimamia Vyama hivyo.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Queen Sendiga katika ufunguzi wa mafunzo hayo amewataka Maafisa Ushirika baada ya mafunzo hayo watoke wakiwa na uelewa mzuri wa namna ya kusimamia Vyama pamoja na kuondoa baadhi ya changamoto zinazoikabili Sekta ya Ushirika nchini.



***Baadhi ya Wadau wa Ushirika walioshiriki ufunguzi wa mafunzo kwa Maafisa Ushirika yaliyofanyika Mkoani Mtwara***

## KIKAO CHA WADAU KUJADILI MAPENDEKEZO YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA NA.6 YA MWAKA 2013

Kikao cha Wadau Kujadili Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 kilifanyika tarehe 17/09/2021 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Benki Kuu, Jijini Dar Es Salaam na kufunguliwa na Waziri wa Kilimo, Mhe. Prof. Adolf Mkenda akiambatana na Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, Kikao hicho kilihusisha Wadau Wazoefu wa Ushirika: Bw. Paul Kimiti, Pius B. Ngeze, Stephen Safe, Emmanuel Malunde, Joseph Mihangwa, Hasan Wakasuvi, Mhe Balozi. Dkt. Ladislaus Komba, Dkt. Florens Turuka, Dkt. Audax Rutabanzibwa, Dkt. Jones Kaleshu na Dkt. Anaclet Kashuliza.



*Waziri wa Kilimo Mhe. Prof. Adolf Mkenda, akifungua Kikao cha Wadau Kujadili Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013*



*Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, akizungumza katika Kikao cha Wadau Kujadili Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013*



***Baadhi ya Washiriki wa Kikao cha Wadau Kujadili Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013***

## USHIRIKA WATAKIWA KUJIENDESHA KISASA NA KUGUSA MAKUNDI YOTE

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Dkt.Benson Ndiege, amevitaka Vyama vya Ushirika nchini, kujiendesha kisasa ikiwa ni pamoja na kuwa na ushirika wenye kugusa makundi yote, vijana, wazee, kina mama na wafanyakazi wa makundi yote.

Dkt. Ndiege amesema Tume imedhamiria kuimarisha zaidi matumizi ya Mifumo ya Kieletroniki katika ukusanyaji wa taarifa mbalimbali ambazo zitasaidia Ushirika kujiendesha kisasa. Mrajis ameyasema hayo Septemba 10, 2021, jijini Dodoma wakati wa Kikao kazi cha wadau wa ushirika kutoka mikoa mbalimbali nchini wakati wa mapitio ya Mpango Mkakati wa Tume, ambapo amesema kwa sasa ni lazima kuwe na Ushirika wa kisasa na kuachana na uendeshaji wa Ushirika kwa mazoea.

“Lazima tubadilike tuwe na ushirika ambao unawagusa vijana, wazee kina mama na wafanyakazi na makundi yote; wavuvi, Waandishi wa Habari, lazima tusibaki na ushirika wa kizamani hata mifumo yetu lazima iende kisasa. Wewe kama unaendelea kutembelea na makaratasi wenzako wapo kwenye simu wanapata information lazima na sisi tuendane na hali halisi ya nchi yetu jinsi ilivyo,”amesema Dkt. Ndiege

Aidha, Dkt. Ndiege amesema ili Ushirika uweze kwenda vizuri ni lazima kuwe na imani kwa kile ambacho kinafanyika ambapo watu wasipokuwa na imani ni sawa na kazi bure. “Kwa sasa tunachotamani kwa ukubwa ni imani katika vyama vya ushirika watu wasipokuwa na imani hata tupige kelele au tuweke mifumo gani hawatatumia fursa hizo.Unaweza ukaenda kijijini ukapiga shule yako wanakusikiliza wanakwambia miaka kumi chama chetu kilikuwa kinaleta pembejeo lakini sasa hivi hakuna.



***Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege akifungua kikao cha Wadau wa Tume kujadili Mpango Mkakati wa Tume, Jijini Dodoma***

“Hatuwezi kwenda bila kuleta imani hili ni jukumu letu sote lazima tuanze kwa kujenga imani kwa kuwa waaminifu,” amesema Dkt.Ndiege

Amesema malengo yao ni kuhakikisha kunakuwa na vyama imara vya ushirika ikiwemo kuviona vyama hivyo vinakuwa na mifuko ya pembejeo ili viweze kujitegemea.

“Ni bora kuwa na vyama vichache na sisi tunajikita na kuwa na vyama imara vya ushirika kwa sababu hiyo tunayo malengo ambayo yatasaidia vyama, mojawapo kwenye vyama vya mazao tungependa kuona vyama hivyo vinakuwa na mifuko ya pembejeo na sisi tutajenga mazingira ili jambo hili liende vizuri,” amesema Dkt. Ndiege

“Tumejikita zaidi kuingia katika mifumo ya kieletroniki katika vyama vya ushirika na tayari zoezi hili limeanza na tutatunza taarifa vizuri na tunawaalika wadau kulifanikisha hili. Tunataka mifumo ioneshe wameingia wanachama wangapi na wamepata pembejeo kiasi gani,” amesema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC), Theresia Chitumbi amesema Mkutano huo upo kwa ajili ya kuGandaa ushirika mpya ambao utaenda kisasa.

“Tupo hapa kuandaa mikakati ya Tume ya Ushirika kwani ni wadau wa ushirika tupo kwa ajili ya kuleta ushirika mpya na hilo ndilo lengo la Rais wetu na tumeona nchi nyingi ambazo ushirika umesimama ndio wana maendeleo makubwa,”amesema

Amesema Ushirika wa zamani ulikuwa wa mazao tu lakini sasa hivi wamejipanga kuwavuta vijana na kuubadilisha ushirika na uwe wa kidigitali.

“Mimi kwa mtazamo wangu tunatakiwa kubadilika tuwe na ushirika wa kidigitali kuliko kwenye makatarasi ukiwa kidigitali kila kitu kinaonekana tumeanza kuwaingiza vijana,”amesema.



***Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika Bw. Collins Nyakunga akifafanua jambo kwa wadau wa Tume ya Maendeleo wakati wa kujadili mkakati wa Tume, Jijini Dodoma***



***Wadau wakifuatilia mijadala kuhusu Mpango Mkakati wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika***

## WARAJIS WASAIDIZI WATATU WABADILISHIWA VITUO VYA KAZI, MMOJA ATEULIWA

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amefanya mabadiliko kwa kuwahamisha vituo vya kazi Warajis Wasaidizi watatu na kumteua Afisa Ushirika mmoja kuwa Kaimu Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika.

Warajis Wasaidizi waliohamishwa vituo vya kazi ni Emmanuel Sanka, aliyekuwa Mrajis Msaidizi Mkoa wa Arusha, ambaye amehamishiwa makao makuu ya Tume kuwa Mrajis Msaidizi anayesimamia masuala ya Sheria na Usajili; Angela Maganga aliyekuwa Mrajis Msaidizi mkoa wa Mbeya, amehamishiwa Mkoa wa Singida kuendelea na Wadhifa wake; na Grace Msambaji, aliyekuwa Mrajis Msaidizi Mkoa wa Singida, amehamishiwa Mkoa wa Arusha kuendelea na Wadhifa wake.



Angela Maganga,
Mrajis Msaidizi
Mkoa wa Singida




Emmanuel Sanka,
Mrajis Msaidizi
Sheria na Usajili



Grace Msambaji,
Mrajis Msaidizi
Mkoa wa Arusha

Aidha, Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania amemteua Richard Zengo, kuwa Kaimu Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Mbeya. Kabla ya kuteuliwa kwake kuwa Mrajis Msaidizi, Zengo alikuwa Afisa Ushirika mkoani Lindi.



Richard Zengo,
Kaimu Mrajis Msaidizi
Mkoa wa Mbeya


TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA
TANZANIA (TCDC)
NAMBA ZA SIMU ZA TUME YA MAENDELEO
YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)
0800110105
Maulizo na ushauri:
Piga 0735 032 348,
0735 032 349
au
Piga simu bure(Toll-Free)
0800110105,
0800110109
www.ushirika.go.tz
ushirika@ushirika.go.tz
ushirika_tcdc
@ushirika_tcdc
Tume ya maendeleo ya ushirika

# WITO WATOLEWA USHIRIKA KUONGEZA KASI YA VIWANDA

Wito umetolewa kwa Vyama vya Ushirika kuangalia namna bora ya kuendeleza viwanda vinavyochakata bidhaa zinazozalishwa na Vyama vya Ushirika kwa kuongeza thamani ya mazao mbalimbali yanayotoka na vyama hivyo ili kuweza kuendana na kasi ya soko la ushindani la ndani na nje ya nchi.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Kilimo Mhe. Prof. Adolf Mkenda wakati akifungua Kongamano la Pili la Kimataifa la Ushirika katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) mkoani Kilimanjaro. Kongamano liliandaliwa kwa ushirikiano wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), na lilianza Septemba 01, 2021 hadi Septemba 03, 2021 na. Kaulli mbiu ya Kongamano ilijikita katika masuala ya Ushirika na Maendeleo ya Viwanda kwa kuzingatia maslahi ya wanachama.

Waziri alieeleza kuwa ni dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita kuona Vyama vya Ushirika vinaongeza tija kwa kuongeza viwango vya uzalishaji ili iwe ni msukumo wa kuanzisha na kuendeleza Uchumi wa Viwanda kwa kuongeza thamani ya mazao na bidhaa zinazotokana na Vyama, ingawa bado Sekta ya Ushirika inakabiliwa na changamoto zinazopaswa kufanyiwa kazi.

“Lengo la Serikali ni kuimarisha na kuendeleza Ushirika ingawa ushirika unakabiliwa na changamoto za Kisera, masuala ya Sheria, hitaji la wataalamu katika utendaji wa Vyama vya Ushirika,” alisema Prof. Mkenda

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege katika Kongamano hilo alisema Tume kwa mujibu wa Sheria Na.6 ya mwaka 2013 itaendelea kutekeleza wajibu wa kuvisimamia na kuhamasisha Vyama vya Ushirika.

“Ni wakati sasa Vyama vya Ushirika vifikirie kuwa na viwanda vya kuchakata mazao mbalimbali na kuyaongezea thamani ili kuzalisha bidhaa zinazotokana na maziwa, asali, alizeti na mengine mengi,” alieleza Mrajis

Mrajis ameongeza kuwa hivi sasa Sekta ya Ushirika ina viwanda mbalimbali 452 ambavyo vinafanya shughuli mbalimbali za uchakataji. Akibainisha juhudi zinazoendelea katika kuendeleza na kuimarisha viwanda vya Ushirika ni pamoja na uanzishaji wa Kiwanda cha vifungashio katika Chama cha Ushirika SONAMCU mkoani Ruvuma, kiwanda cha ubanguaji Korosho TANECU mkoani Mtwara, Kiwanda ambacho kimeanza kazi ya kuchambua Pamba mkoani Shinyanga kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahawa (KACU) pamoja na vingine.

Akichangia mada wakati wa Kongamano hilo Mtaalamu wa Uchumi Prof. Honest Ngowi ameshauri Vyama vya Ushirika vingi kwa sasa vinazalisha bidhaa na mazao yakiwa ghafi jambo ambalo bado linafanya tija na uchumi wa Vyama kuwa duni.

Aliongeza kuwa uuzaji na usafirishaji wa mazao yaliyoongezwa thamani nje ya nchi unachangia kuongeza pato la Taifa, fursa za ajira, na uchumi wa mtu mmoja mmoja ambao hatimaye utachangia kupunguza umaskini. Akibainisha kuwa hadi kufikia 2020 Viwanda vinachangia ajira kwa kiasi cha asilimia 40. Jambo ambalo likiimarishwa litainua uchumi hasa wa Sekta binafsi na hatimaye Taifa kwa ujumla.

Akichangia mada wakati wa Kongamano hilo Mtaalamu wa Uchumi Prof. Honest Ngowi ameshauri Vyama vya Ushirika vingi kwa sasa vinazalisha bidhaa na mazao yakiwa ghafi jambo ambalo bado linafanya tija na uchumi wa Vyama kuwa duni.

Aliongeza kuwa uuzaji na usafirishaji wa mazao yaliyoongezwa thamani nje ya nchi unachangia kuongeza pato la Taifa, fursa za ajira, na uchumi wa mtu mmoja mmoja ambao hatimaye utachangia kupunguza umaskini. Akibainisha kuwa hadi kufikia 2020 Viwanda vinachangia ajira kwa kiasi cha asilimia 40. Jambo ambalo likiimarishwa litainua uchumi hasa wa Sekta binafsi na hatimaye Taifa kwa ujumla.

Aidha, Mtaalamu huyo wa uchumi ameeleza kuwa wigo mpana wa Vyama vya Ushirika kushiriki katika uchumi na maendeleo ya viwanda kutokana na dhana ya ushirika kuwa yenye uwezo wa kushirikisha Nyanja mbalimbali za uchumi ikiwemo vyama vya ushirika wa kilimo, uvuvi na maeneo mengine.

Pamoja na mambo mengine uzinduzi wa Kongamano hilo ulienda sambamba kwa utiaji saini wa mikataba ya Ushirikiano baina ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, MoCU na Bodi ya Kahawa, MoCU na Shirikisho la Vyama vya Akiba na Mikopo (SCCULT).

Mada zilizojadiliwa katika Kongamano hilo ni pamoja na masuala yanayohusu namna bora ya kuongeza uweledi katika utendaji wa vyama, Hifadhi ya Jamii kwa wanaushirika, mabadiliko na maboresho ya Sheria za Ushirika, Ushirikishwaji wa Vijana katika Vyama vya Ushirika zote zikilenga kujadili changamoto ili kupata mapendekezo ya suluhu za kuboresha Sekta ya Ushirika.




***Waziri wa Kilimo Mhe. Prof. Adolf Mkenda akiongea na Wanaushirika wakati wa Kongamano la Pili la Kimataifa la Ushirika lililofanyika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Kilimanjaro***




***Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege (kulia), Makamu Mkuu wa Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU) Prof. Alfred Sife (kushoto) kwa pamoja wakionesha Mkataba wa ushirikiano baina ya Taasisi hizo, katikati akishuhudia ni Mwanasheria wa Tume Bw. Shani Mayosa***



***Wadau mbalimbali wakifuatilia majadiliano wakati wa Kongamano la Pili la Kimataifa la Ushirika, Moshi Kilimanjaro***

## KAMATI MAALUM YA BUNGE YAFANYA ZIARA KATIKA MIKOA YA RUVUMA, LINDI NA MTWARA ILI KUJIFUNZA NAMNA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA UNAVYOTEKELEZWA

Kutokana na faida zilizobainishwa katika matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala nchini, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliteua Kamati maalum yenye wabunge wanne (4) ambao ni Mhe. Rashid Shangazi (Mbunge wa Mlalo), Mwenyekiti, Mhe. Kunti Majala (Mbunge Viti Maalum, Dodoma), Mhe. Denis Londo (Mbunge wa Mikumi) na Mhe. Jackson Kiswaga (Mbunge wa Kalenga) wakiwa wajumbe.



***Mhe. Rashid Shangazi (Mbunge wa Mlalo), Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Bunge akizungumza katika kikao na Wakulima/ Wanaushirika (hawapo pichani)***

Kamati hiyo iliongozwa na Mhe. Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mh. Exaud Kigahe akiwa mwenyeji na mwenye dhamana juu ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara. Aidha, Kamati iliambatana na wakuu wa Taasisi ambao ni Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Vipimo (WMA) na Mkurugenzi wa Biashara,Wizara ya Viwanda na Biashara.



***Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe akizungumza katika kikao na Wakulima/ Wanaushirika (hawapo pichani) wakati wa ziara ya Kamati Maalum ya Bunge***

Lengo la Kamati hiyo maalum ni kujifunza namna ya mfumo huu unavyofanya kazi kwa kuangalia faida na changamoto. Kamati ilifanya ziara ya mafunzo tarehe 22 – 27 Septemba, 2021 na kupita katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Namtumbo, Tunduru, Masasi, Nachingwea, Ruangwa na Lindi katika mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara ikiwa ni maeneo ambayo mfumo wa Stakabadhi za Ghala unatekelezwa.



***Baadhi ya Washiriki katika ziara ya Kamati Maalum ya Bunge***



***Mmoja wa wakulima akizungumza katika kikao wakati wa ziara ya Kamati Maalum ya Bunge***

## SHIRIKA LA *USADF* LIMETOA SHILINGI MILLIONI 231.6 KWA USHIRIKA WA WAKULIMA WA MAPARACHICHI, RUNGWE

Shirika la ***USADF COUNTRY PROGRAM*** kutoka nchini Marekani limetoa kiasi cha shilingi 231,612,800/= kwa Ushirika wa Wakulima wa Maparachichi Rungwe (UWAMARU) kwa ajili ya kuboresha zao hilo kwa kipindi cha miaka miwili.

Akizungumza mara baada ya kuwekeana mikataba na ushirika huo, Meneja wa Program USADF hapa nchini, Gillian Nkini, amesema fedha hizo zitatumika katika kuboresha kilimo cha Maparachichi.

Amesema kuwa fedha hizo zitatengwa kwa ajili ya kusaidia pembejeo kwa wakulima, kuwawezesha wakulima kimafunzo, kutembelea ushirika mwingine katika mikoa ya Njombe na Kilimanjaro.



***Shirika la USADF COUNTRY PROGRAM na Ushirika wa Wakulima wa Maparachichi Rungwe (UWAMARU)wakikabidhiana Mkataba wa Makubaliano.***

Nkini amesema mradi huo pia utawezesha kununua vifaa mbambali ikiwemo kompyuta, pikipiki, magari pamoja na mafunzo ya kusimamia matumizi ya fedha.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa hafla hiyo Mkuu wa wilaya ya Rungwe, Dkt. Vincent Anney ameutaka Ushirika huo kuwa na umoja na kutumia pesa hizo kwa malengo na kuwashirikisha wakulima.

Anney amesema kuwa Maafisa Ushirika wanapaswa kutokuwa chanzo cha migogoro ndani ya Ushirika na badala yake kuhakikisha wanatoa mafunzo na maelekezo yatakayowezesha kusimamia utekelezaji amesema lazima jicho lake liwe kwa ushirika wa wakulima hao huku akiwataka kutumia mradi huo pia katika kuendeleza mazao mengine.

Mwenyekiti wa UWAMARU, Bw.Kayusi Msigwa akizungumzia fedha hizo amesema licha ya kuleta tija na kubadilisha sura ya uendeshaji kwa wakulima amesema Ushirika hautovumilia kuona bado wakulima wanalima kwa mazoea na kuvuna parachichi zisizokomaa. Msigwa ameiomba Halmashauri ya Rungwe kuendelea kusimamia wakulima juu ya wizi unaofanywa na walanguzi wa parachichi hatua ambayo anasema inaweza kuleta taharuki kwa pande zote mbili.

Kwa upande waMrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Mbeya, Angela Maganga, amewataka viongozi wa Ushirika huo kusimamia Sheria na taratibu kwa matumizi ya pesa watakazopatiwa ili Ushirika mwingine ujifunze kutoka kwao.

## VYAMA VYA USHIRIKA NA MAAFISA USHIRIKA MKOANI RUKWA WAPATA VITENDEA KAZI

Shirika lisilo la kiserikali HELVETAS International na BRiTEN kwa pamoja wamekabidhi mizani 4 kwa Vyama vya Ushirika na Simu Janja (Tablets) kwa Vyama vya Ushirika 19 na Maafisa Ushirika sita (6) wa Mkoa wa Rukwa. Vifaa hivi vitasaidia Vyama vya Ushirika kutunza kumbukumbu kidijitali na kuweza kupata taarifa kwa Urahisi.



Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Rukwa, Bw. Benjamin Mwangwala amesema vifaa hivi vilikabidhiwa na Bi.Macrina Saimon, Afisa Tathmini na Ufuatiliaji wa Taasisi ya BRiTEN tarehe 20/9/2021 katika Ukumbi wa Mkuu wa Mkoa Rukwa .

Mheshimiwa Joseph Mkirikiti, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa katika mkutano wake wa kwanza na viongozi wa Vyama vya Ushirika pamoja na mambo mbalimbali, alielekeza kwa Mrajis Msaidizi Mkoa Rukwa kuangalia namna ya kuwa na kanzi data ya Ushirika ya Mkoa wa Rukwa. Hivyo, kwa ushirikiano uliopo kati ya Ofisi ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Mkoa wa Rukwa, Shirika lisilo la kiserikali HELVETAS International na BRiTEN kwa pamoja waliweka mkakati wa utekelezaji wa muda mfupi.

Aidha, tarehe 8 Septemba, 2021 wakati wa ziara ya ugeni wa DANIDA, suala la mashirikiano yanayoendelea ngazi ya Mkoa yalipewa kipaumbele. Pamoja na ushuhuda wa mafanikio yaliyopo ikiwa ni pamoja na MPUI AMCOS Ltd kuwa na website yao na uwezo wa kuajili mtendaji na pia ushawishi wa kupata tender ya kuiuzia WFP mahindi, upungufu wa Mizani ngazi ya AMCOS na kutokuwa na kanzi data ya Ushirika Mkoa wa Rukwa vilipewa umuhimu stahiki.

"Ugeni huo ulizichukua changamoto hizo na nyingine na Ofisi ya Mrajis Msaidizi pamoja na Meneja wa Shirika la HELVETAS International Rukwa na Mwakilishi wa BRiTEN walianza ufuatiliaji kwa ukaribu. Hatimae matunda sasa yanaanza kuonekana. Shime wanaushirika wa Mkoa wa Rukwa," amesema Mwangwala.

## MNADA WA KWANZA WA MBAAZI TUNDURU WAINGIZA SHILINGI 466,623,690.00

Mnada wa kwanza wa mauzo ya Mbaazi Wilayani Tunduru katika Mkoa wa Ruvuma uliofanyika tarehe 12 Agosti, 2021 kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ambapo mnada huo ulifanyika Kijiji cha Mtonya katika chama cha Msingi Mtetesi Wilayani Tunduru na jumla ya fedha zilizokusanywa kupitia mnada huo ni Shilingi 466,623,690.00.

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Ruvuma, Bumi Masuba, amesema jumla ya kilo zilizokuwa sokoni leo ni 360,351 na bei ya wastani kwa mkulima imekuwa Shilingi 1,294.16 kabla ya tozo. Aidha, wanunuzi walinunua kwa mchanganuo ufuatao: Mohammed Enterprise kilo 150,000 kwa bei ya Shilingi 1,300 sawa na Shilingi 195,000,000.00; RBST International kilo 210,251 kwa bei ya Shilingi 1,290 sawa na Shilingi 271,623,690.00 na hivyo kufanya jumla ya fedha zilizoingia Tunduru kuwa Shilingi. 466,623,690.00.



***Wakulima  Wa Mbaazi wakishiriki Ufunguzi wa Sanduku la Mnada uliofanyika Wilayani Tunduru***

Jumla ya tozo kwa mkulima ni Shilingi 52 mbali na usafiri kutegemeana na umbali kwa kilomita. Hivyo, katika kila kilo moja (1) Mkulima anapata zaidi ya Shilingi 1,200 moja kwa moja kwenye akaunti yake.

Mnada huu unaondoa propaganda kwamba Mkoa wa Ruvuma umeamua Mbaazi zinunuliwe kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ili kumuumiza mkulima kwa kuwa wakulima waliohadaiwa na kukubali kuuza Mbaazi zao kwa mfumo wa Walanguzi, wameambulia kuuza kwa bei kati ya Shilingi 300 hadi 600 kwa kilo 1 ya Mbaazi.

Huu ni ushahidi mwingine ya kwamba, mazao yanapouzwa kwa Stakabadhi za Ghala, mkulima anasogezewa soko la moja kwa moja la Wanunuzi wakubwa ambao hutegemewa pia na Walanguzi wanaonunua kwa wakulima.

Viongozi wa Mkoa wa Ruvuma akiwemo Mkuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya za Mkoa huo wanastahili pongezi kwa kuendelea kumtetea mkulima wa Ruvuma kwa usimamizi wao madhubuti.




***Wakulima wakiwa katika Mnada wa kwanza wa Mbaazi Wilayani Tunduru***

# MAKALA ZA USHIRIKA WA NYUMBA

## NJIA ZA MIIBUKO YA VYAMA VYA USHIRIKA WA NYUMBA

**Ndugu Msomaji wa Jarida la Ushirika,** karibuni tena katika makala za Ushirika wa nyumba. Katika toleo lililopita tuliangalia mchango wa Vyama vya Ushirika wa Nyumba kufikia azma ya nyumba kwa wote na ukuaji wa Miji. Katika toleo hilo tulijieelekeza katika kuangalia umuhimu wa Vyama vya Ushirika wa Nyumba katika mnyororo wa Thamani, Ushirika wa Nyumba na malengo ya maendeleo endelevu.

katika toleo hili tunakwenda kuangalia **Njia za Miibuko ya Vyama vya Ushirika wa Nyumba.** Kwa ujumla tunaangalia namna ambavyo Vyama vya Ushirika wa Nyumba vinaweza kutokea au kuwepo na hatimaye kusajiliwa na kuweza kuendesha shughuli zake. Vyama vya ushirika wa nyumba vinaweza kuanzishwakutokana na njia tano ambazo zinaitwa njia za miibuko ya Vyama vya Ushirika wa Nyumba. Hivyo, vyama vya ushirika wa nyumba vilivyopo hapa nchini vilianzishwa kutokana na baadhi ya njia zilizooneshwa kwenye mchoro hapa chini.




***Mchoro: Miibuko ya Vyama vya Ushirika wa Nyumba***

**Njia za uatamizi**

**Ndugu Msomaji wa Jarida la Ushirika,** Njia ya uatamizi inahusisha Vyama vya Ushirika wa Nyumba ambavyo uwepo wake hutokana na miradi iliyokuwa chini ya ufadhili wa taasisi ambazo siyo za kiushirika. Taasisi hizo zinaweza kuwa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO), miradi ya Serikali au Mashirika ya Umoja wa Mataifa.

Suala la msingi katika njia ya uatamizi ni kwamba wakati miradi ya nyumba inaanza; lengo la wahusika inakuwa siyo kuanzisha Chama cha Ushirika wa Nyumba ambacho kinaweka mikakati ili kuwezesha wanachama wake kupata nyumba.

Mara nyingi taasisi hizo zinakuwa na mipango au miradi ya kuwezesha wananchi wa kipato cha chini kupata makazi. Wakati ambapo jitihada za kuwezesha wananachi zinapokuwa zinaendelea, ndipo wazo la kuunda Ushirika wa Nyumba hujitokeza kupitia kwa wafadhili wa miradi hiyo. Hivyo, wahusika kulazimika kuanzisha Chama cha Ushirika wa Nyumba pengine kama njia mojawapo ya kuhakikisha kuwa afua (intervention) za mradi zinakuwa endelevu.

Dhana ya **uatamizi** inajitokeza wakati ambapo Chama cha Ushirika wa Nyumba kinaanzishwa na kinaendelea kulelewa na mradi husika. Wakati mwingine watumishi wa mradi ndio wanaweza kuwa watumishi wa Chama cha Ushirika wa Nyumba na hata wanaweza kulipwa mishahara na mradi. Chama cha Ushirika wa Nyumba kinaweza kuwa kinapata msaada wa kujengewa jengo la ofisi na mradi, kupewa vifaa vyote vya ofisi kama vile Shajala, Komputa, Samani za ofisi, Sefu n.k. Hali hiyo inaweza kuendelea hadi wakati ambapo mradi unamaliza muda wake, ndipo Chama cha Ushirika wa Nyumba kinaweza kuachiwa ili kiweze kuendesha shughuli zake chenyewe.

**Changamoto za njia ya Uatamizi**

Ndugu Msomaji wa Jarida la Ushirika, ikumbukwe kwamba kila njia ya mwibuko wa Ushirika wa Nyumba ina manufaa na changamoto zake kutegemea jinsi watu walivyoanza. Katika toleo hili tunakwenda kuangali hasa changamoto zinazojitokeza kupitia njia ya uatamizi.

Changamoto kubwa ya njia ya uatamizi ni wanaushirika kupata ugumu katika kufuata taratibu za usimamizi wa Vyama vya Ushirika kama vile kuitisha mikutano kwa mujibu wa masharti yao, uandaaji wa makisio ya mapato na matumizi na kufanya ukaguzi wa nje wa hesabu za chama. Hii inatokana Chama kuanzishwa chini ya usimamizi wa mradi kupitia Shirika au taasisi ambayo iliyofadhili fedha zote za mradi na uendeshaji wa Chama cha Ushirika wa Nyumba kwa kuwa Chama kinakuwa ni sehemu ya mradi. Hivyo, wakati mwingine inakuwa ni vigumu kufuata taratibu za kiushirika.

Ili kukabiliana na changamoto hii taasisi zenye miradi inayoatamia Chama cha Ushirika wa Nyumba inapaswa kuhakikisha kuwa Wanachama wanajengewa uwezo katika maeneo mengi, hususani katika masuala ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika, vingenevyo inaweza kutokea Chama cha Ushirika wa Nyumba chenye vazi la Ushirika kwa maana ya kuandikishwa kwa Sheria ya Vyama vay Ushirika, lakini uendeshwaji wake haufuati misingi ya ushirika.

Suala jingine ni kuhakikisha kuwa Mamlaka za usimamizi wa Vyama vya Ushirika zinakuwa karibu na vyama hivi kwa kuwaelekeza na kuwapa ushauri ili wakati mradi unamaliza muda wake, wasimamizi wa Ushirika waweze kuendelea kukilea chama cha Ushirika kwa karibu zaidi.

**Ndugu Msomaji wa Jarida la Ushirika,**katika toleo lijalo tunaendelea kuangali mifano mbalimbali ya Vyama vya Ushirika wa Nyumba vilivyoko hapa nchini ambavyo vimetokana na njia ya uatamizi.

**Mwandishi:-**
Mwandishi wa Makala hii ni Afisa Program, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, (MoCU), Ofisi ya Dodoma.
Simu: +255 764 021 915

## USHIRIKI WA TCDC KATIKA MAONESHO YA BIASHARA YA 45 YA SABASABA PICHANI- DAR ES SALAAM




***Muonekano wa Banda la Tume ya Maendeleo ya Ushirika wakati wa Maonesho ya Biashara ya 45 ya Sabasaba Mkoani Dar es salaam***



***Maafisa Ushirika kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika wakisikiliza kwa makini maelezo yanayotolewa na mdau aliyetembelea banda la Tume katika maonesho ya Sabasaba***




***Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) akisaini kitabu cha wageni katika Banda la Tume, wakati wa Sabasabat***




***Mrajis Msaidizi wa Mkoa wa Dar es salaam Bw. Abdilahi Mtabazi Pamoja na Afisa Ushirika Bw. Ndimolwo Laizer wakimsikiliza kwa makini mdau aliyetembelea banda la Tume wakati wa maonesho ya Sabasaba***

## USHIRIKI WA TCDC KATIKA MAONESHO YA 16 YA BIASHARA YA AFRIKA MASHARIKI- MKOANI MWANZA



*Afisa Ushirika Bw. Aron Mrema akifafanua jambo kuhusu Ushirika wakati wa Maonesho ya 16 ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Mkoani Mwanza*



*Maafisa Ushirika wakishirikiana na Wadau wa Ushirika wakitoa huduma na elimu ya Ushirika wakati wa Maonesho ya 16 ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Mkoani Mwanza*




*Afisa Ushirika Bi. Elizabeth Muzo akielezea masuala ya Ushirika wakati wa Maonesho ya 16 ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Mkoani Mwanza*



*Wadau mbalimbali wakijifunza kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanyika katika Vyama vya Ushirika wakati wa Maonesho ya 16 ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Mkoani Mwanza walipotembelea Banda la Tume ya Maendeleo ya Ushirika.*

*Limetolewa na*

**Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)**
Mtaa wa Kuu, S.L.P. 201, DODOMA.

Simu: +255 26 23 22456, Telefax: +255 26 23 21973

B.Pepe: **ushirika@ushirika.go.tz** Tovuti: **www.ushirika.go.tz**